**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**

**SHULE YA SEKONDARI NYUMBU**

**MTIHANI WA ROBO TATU MUHULA KIDATO CHA TATU**

**MSIMBO: 021** **KISWAHILI**

**MUDA: MASAA 3** **AGOSTI, 2023**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu A, B, na C wenye jumla ya maswali **kumi na moja (11).**
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na B maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C swali la 11 ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama 16, sehemu B ina alama 54 na sehemu C ina alama 30
4. Simu za mikononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani
5. Zingatia maelekezo ya kila sehemu ya kila swali.
6. Andika **Namba Yako ya Mtihani** kwenye kila kurasa wa karatasi ya kujibia.

**SEHEMU A ( ALAMA 16)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele **(i) – (x),** kisha andika herufiya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.
   i) Mwamvita ametunga sentensi yenye aina mbalimbali za maneno,unadhani katika sentensi hiyo ni neon lipi kati ya hayo linaweza kudokeza mtenda au mtendwa ?
   A. Kiunganishi C. Kihisishi E. Kielezi
   B. Kivumishi D. Kiwakilishi
   ii) Miongoni mwa sifa za kitenzi kisaidizi (Ts) kutoweza kutoa taarifa kamili, ukiwa kama mtaalamu wa sarufi, bainisha sentensi ambayo **haina** kitenzi kisaidizi
   A. Mwalimu wetu alikuwa mtiifu sana
   B. John alikuwa anasoma kitabu cha hadithi nzuri
   C. Paka alikuwa anataka kula chakula cha mbwa wetu
   D. Watoto wanatakiwa kulala mapema ili wawahi shuleni
   E. Ngoswe Mitomingi anataka kuja kutumbuiza mwezi Desemba.
   iii) Katika kazi ya fasihi kuna wahusika ambao hawabadiliki na kupewa majina ambayo humfanya msomaji aelewe tabia na matendo yao. Je wahusika hao wanaitwaje?
   A. Wahusika duara C. Wahusika bapa
   B. Wahusika wakuu D. Wahusika shinda
   E. Wahusika wajenzi
   iv) Ndizi **za Moshi** ni tamu sana. Neno lililopigiwa mstari ni aina gani ya neno?
   A. Kivumishi C. Kiakilishi E. Kielezi
   B. Kiunganishi D. Nomino
   v) Mwalimu Jenesta amewapa wanafunzi wake kazi ya darasani, ya kutunga hadithi, hadithi hiyo inatakiwa kuonesha historia ya vita ya maji maji iliyotokea Songea. Je, hadithi hiyo itakuwa katika kipera gani?
   A. Ngano C. Tarihi E. Soga
   B. Kisasili D. Majigambo
   vi) kwenye mazungumzo ya Aisha na Mama yake, Aisha alisikika akimueleza mama yake kuwa, ‘’Nilikwenda kwa Shangazi nikamkuta hayupo.’’ Je, Aisha amefanya makossa gani kati ya haya yafuatayo:-
   A. Kimantiki C. Kimuundo
   B. Kimsamiati D. Kuongeza vitamkwa
   E. Kimaana
   vii) Utata katika mawasiliano ni hali ya neno au sentensi kuwa na maana Zaidi ya moja. Ili kuepuka utata huo, ni jambo gani muhimu la kuzingatia kati ya yafuatayo:-
   A. Kuzingatia kiwango cha msikiko wa sauti katika utamkaji
   B. Utaratibu maalumu wa kushusha na kupandisha mawimbi ya sauti
   C. Kuepuka kutumia maneno na tungo zenye maana Zaidi ya moja
   D. Kutumia vitendawili na methali
   viii) Mtumiaji wa lugha ya Kiswahili anapotamka baadhi ya silabi kwenye neno huongeza nguvu katika kutamka kuzidi nyingine, hali hiyo huitwaje?
   A. Kiimbo C. Lafudhi E. Umbo sauti
   B. Mkazo D. Fonimu
   ix) Ukiwa kama mtaalamu wa Sarufi, unadhani ni mpangilio upi ni sahihi wa vipashio vinavyounda lugha ya Kiswahili

A. Mofimu, kishazi, kirai, neno na sentensi B. Mofimu, neno, kirai, sentensi na kishazi
B. Mofimu, neno, kirai, sentensi na kishazi
C. Neno, kirai, kishazi, sentensi na mofimu
D. Neno, mofimu, kirai, kishazi na sentensi
E. Mofimu, neno, kirai, kishazi, na sentensi

x) Nyimbo ziimbwazo na wakulima wakati wakiwa katika shughuli zao za kilimo ili kuwatia hamasa huitwa

A. Kimai
B. Wawe
C. Dondozi
D. Mashairi
E. Tendi

2. Oanisha maana ya dhana ya vifungu vya maneno vilivyo katika **orodha A** kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika **Orodha B,** kisha andika herufi ya jibu husika kijitabu chako cha kujibia

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| i) Lugha inayozungumzwa na watu wenye asili ya lugha mbili tofauti | A. Chagizo |
| | B. Pijini |
| ii) Lugha ya kibantu | C. Krioli |
| iii) Muunganiko wa lugha za makabila tofauti zenye kufanana | D. Kiswahili |
| iv) Lugha iliyounganika kati ya kiarabu na Kiswahili | E. Shamirisho |
| v) Sehemu ya kiarifu inayokaliwa na nomino | F. Kiarabu |
| vi) Lugha inayotokana na ukomavu wa pijini | G. Kibantu |
| | H. Chotara |
| | I. Lahaja |

## SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Mmepewa kazi na Mwalimu wenu wa somo la Kiswahili kuhusu dhana ya kirai. Ukiwa kama mmoja wa wanafunzi hao, uliyeshiriki mjadala huo. Fafanua aina tano za virai (kila moja thibitisha kwa mfano bayana)
4. Juma amekuwa ni mtu wa kutumia lugha ya matusi, kejeli na isiyosanifu kwa wanakijiji wenzake, unadhani chanzo cha kutumia lugha hiyo ni kipi? (toa hoja sita na zenye mfano)
5. ''Pamoja na Waarabu kuchangia katika kukua na kuenea kwa ligha ya Kiswahili enzi za utawala wao, kulikuwa na mambo yaliyochangia kukidumaza Kiswahili nchini Tanzania''. Tumia hoja nne kuthibitisha dai hilo.
6. Kwa kutumia hoja nne kutoka katika riwaya ya **TAKADINI** onyesha jinsi kazi hiyo ya kifasihi ilivyoweza kuwa mstari wa mbele katika kutetea na kulinda haki za watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali katika jamii zetu.
7. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

''Kweli **<u>vyuma vimekaza</u>**'', huu ni utupu yaani hali yakutokuwa na kitu. Huenda ukawa ni **<u>utupu</u>** **<u>wa pochi</u>**, nyumba, mali, akili na hata utupu wa mwili. Wahenga wa zamani waliwahi kusema mkono mtupu haulambwi. Utupu umegeuka kitu au gumzo la kila siku. Utupu unategemewa kumvusha mtu kutoka sehemu moja kwenye sehemu nyingine.

Tazama nyimbo za Wanamuziki zilivyo. Wasichana wanatumika humo, wanacheza utupu kabisa. Enzi hizo kuonekana mtupu ilikuwa laana kubwa sana. Hali ya mabinti kukaa utupu kwa kiasi kikubwa imepunguza hamu kwa vijana wa kiume kuoa. Ndio, vijana wanaona kila kitu sasa aoe ili iwe nini? Maadili yamebadilika sana kwa sasa. Ni kweli kuwa hapo zamani mwanadamu alitembea utupu, lakini tamaduni hubadilika kulingana na wakati. Mwanadamu tangu kaupata **ustaarabu** wake, utupu sio jambo la kuonesha hadharani.

**Maswali**

i) Pendekeza kichwa cha habari hii kifaacho na kisichozidi maneno matano
ii) Mwandishi ana maana gani anaposema ‘’Mkono mtupu haulambwi”?
iii) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari
iv) Unaelewa nini kuhusu mabinti wa zama hizi? Toa maelezo kwa mistari isiyozidi mitatu (3)

8. Diwani wa kta yenu ya Mkuza ameandaa arambee ya kuchangia ujenzi wa Mabweni katika shule yenu. Kwa niaba ya kamati ya maandalizi, andaa kadi ya mwaliko kuwaalika wadau wa elimu.harambee itafanyika ukumbi wa Destiny Hall Kibaha Pwani, tarehe 20/09/2023. Jina lako liwe Jitihada Zako s.l.p 30849 Kibaha.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii. **Swali la 11 ni lazima**

## ORODHA YA VITABU

***RIWAYA***

- Takadini – Ben Hnson (Mbs)
- Watoto wa mama ntiliye – E. Mbogo (Hp)
- Joka la mdimu A.J. Safari (HP)

***TAMTHILIYA***

- Orodha –Steve Reynolds (Mbs)
- Ngoswe penzi kitovu cha uzembe
- Kilio chetu Medical Aid Foundation.

9. Kwa kutoa hoja tatu kutoka katika riwaya mbili ulizosoma, tumia wahusika wakuu wawili, mmoja kwa kila kitabu kuonesha kukubalika kwao katka jamii ya sasa.
10. ‘’Ujinga na magonjwa ni adui namba moja katika meaendeleo ya taifa lolote duniani” uku ukirejelea vitabu viwili vya tamthiliya ulivyosoma darasani, toa hoja tatu kwa kila kitabu kuonesha umuhimu wa elimu katika jamii yako.
11. ‘’Suala la uwekezaji wa kigeni katika taifa lolote ni jambo muhimu sana. Kwa kutumia hoja nne zenye mashiko andika insha isiyopungua maneno miambili (200) na isiyozdi maneno miambili na hamsini (250) juu ya umuhimu wa uwekezaji wa kigeni kutoka falme za kiarabu (DP WORLD) katika bandari ya Dar es Salaam